# Elimu ya msingi Mji wa Jyväskylä MFANO WA UTENDAJI WA KUPAMBANA NA UONEVU

Kuingilia kati kwenye hali ya uonevu ni jukumu rasmi linalotakiwa kisheria. (Halmashauri ya Elimu)

Wanaoshiriki kwenye elimu wana haki ya kuwa na mazingira salama ya kujifunza. (Sheria ya Elimu ya Msingi 29 §)

Kukubalika na kuheshimiwa

Kuwa sehemu ya jamii, usawa na kuwa na thamani sawa

Mahusiano chanya (positivu)

Mazingira salama na ya kutia moyo

## UZUIAJI ULIOPANGWA KABLA

### 1. Mipango

- Timu itaundwa kwenye kila shule au mtu anayewajibika atateuliwa, ambaye ataratibu na kusimamia kazi ya kupambana na uonevu kwenye kitengo chake. Mtu anayewajibika ni mjumbe kwenye kikundi cha kuhudumia masomo cha jamii.
- Kwenye mpango wa mwaka wa shule mtu anayewajibika kwa kazi ya kupambana na usumbufu, ubaguzi na uonevu, utaratibu wa utendaji, malengo na makadirio anaandikwa kinapomalizika kipindi chake cha utendaji.
- Kanuni zote za utaratibu zinazojulikana na pia mpango wa usawa na kuwa na thamani sawa zinapitiwa kila mwaka pamoja na wanafunzi, walezi na wafanyakazi wote.
- Kwenye mpango wa kuwa na thamani sawa na usawa inabidi kuwa na kanuni za utendaji zilizo wazi, jinsi ya kutengeneza na kusimamia mazingira ya kukubalika na kuheshimiwa.

### 2. Kuimarisha jamii

- Kufahamiana, kujiunga kwenye vikundi na pia kuzuia upweke kutaendelea kwa mwaka wote wa masomo.
- Tunaimarisha kugundua mambo mazuri na kutoa mrejesho chanya kwenye maisha ya kila siku shuleni.
- Kujifunza kuhusu hisia, usalama na ujuzi wa kuwa na mahusiano yamo ndani ya ratiba ya mwaka ya ustawi.
- Tutatumia pia ukaguzi kwa njia ya maswali katika kiwango cha shule, kama vile maswali kwa wanafunzi, maswali kuhusu kuridhika na masomo, maswali kuhusu afya ya shuleni, maswali kuhusu uimarishaji wa afya (TEA), maswali kuhusu ustawi kutoka MLL na pia maswali ya ndani ya darasa, kama sosiogramu (picha ya kuonyesha mahusiano kati ya watu).

## 3. Kutokustahimili uonevu 0

- Kazi ya kupambana na uonevu itaongozwa wazi shuleni.
- Hakuna aina yoyote ya uonevu inayokubalika. Jumuia yote ya shule itaingilia kati kwenye uonevu kwa kizingiti kifupi na kwa utaratibu.
- Wafanyakazi wanapewa uzoefu wa kutosha na mafunzo kuhusu mfano wa hatua za pamoja.
- Wafanyakazi, wanafunzi na walezi wanakuwa makini na kujifunza kutambua mtiririko unaoleta mashaka na dalili za mtu anayeonewa.
- Wafanyakazi wanajipanga kwa kazi ya kupambana na uonevu na kutengeneza mazingira salama shuleni kwa mfano kwa utendaji wa Verso yaani upatanisho kwa watu wa rika moja.

## 4. Utamaduni wa utendaji

- Wanafunzi wanaelewa nini maana ya uonevu, wanajifunza kutambua uonevu na jinsi ya kufanya wakikutana na uonevu.
- Wanafunzi wanatiwa moyo kusema kuhusu uonevu kwa mtu mzima kwa mfano kwa mdomo, kwa kuandika kwenye karatasi bila kutaja jina au kwa njia ya kielektroniki.
- Wanafunzi na walezi wanashiriki kikamilifu kutengeneza utamaduni wa utendaji kupambana na uonevu na kupanga shughuli zinazoongeza moyo wa ushirikiano katika jamii.
- Walezi wanapata taarifa na uwezekano wa kuzungumza kuhusu uonevu, kuweza kutambua uonevu na utendaji wa kupambana na uonevu shuleni.

# KUINGILIA KATI UONEVU

- Wafanyakazi, wanafunzi na walezi wanaweza kushughulikia dalili zinazoonekana kuhusiana na uonevu zinapotokea (kwa mfano kutokufika shuleni, kutokutaka kwenda shuleni, kujitenga, tabia ya ugomvi, "kupiga kofi" ("läpän heitto")).
- Kwanza watu wazima wawili wataongea na aliyeonewa na baada ya hapo wataongea na aliyefanya uonevu, ili kila mwanafunzi aweze kusikilizwa.
- Walezi watapewa taarifa ya yaliyotokea na kuzungumza pamoja nao siku hiyo hiyo.
- Kila tukio la uonevu linaandikwa kwenye kumbukumbu za Wilma kuhusu hali ya uonevu.
- Baada ya kufafanua kuhusu uonevu mwishoni tunawapatanisha na kuandika, jinsi gani tutafanya siku zijazo (tazama kipindi cha ufuatiliaji).
- Ikiwa katika hali ya uonevu kumeshukiwa kuwa na dalili za kosa la jinai, tunawajulisha walezi na kwa kizingiti kifupi tunawasiliana na polisi (kwa mashauriano na polisi wa Ankkuri na mfanyakazi wa ustawi wa jamii, upatanisho).
- Ikihitajika tutatoa taarifa ya ulinzi wa watoto au taarifa ya ulinzi wa watoto na taarifa ya kosa la jinai (kwa mashauriano).
- Uonevu unapotokea njiani wakati wa safari za shuleni tutatoa taarifa kwa walezi na tutatoa msaada wa kufafanua hali hiyo, kwa mfano kuongoza upatanisho.

## KIPINDI CHA UFUATILIAJI NA MSAADA WA BAADAYE

- Hali itafuatiliwa kwa kufuata utaratibu na tutahakikisha uzoefu wa mwanafunzi kwa usalama wa shuleni na safari za shule: Kwa mwezi wa kwanza kila wiki, kwa mwezi unaofuata kila baada ya wiki moja na baada ya hapo kulingana na uhitaji.
- Anayewajibika na ufuatiliaji ni mwalimu wa darasa, kiongozi wa darasa au mtu anayewajibika, ikiwa haikukubaliwa vingine.
- Tutaandaa msaada imara zaidi wa uzuiaji uliopangwa kabla na ufuatiliaji darasani, kwa mfano ujuzi kuhusu hisia na mahusiano, ujuzi wa usalama na ujuzi wa kuwa na marafiki.
- Tutakadiria kuhusu uhitaji wa msaada kwa mwanafunzi aliyefanyiwa uonevu na aliyefanya uonevu na kwa kikundi na ikihitajika tutakubaliana hatua za misaada pamoja na watoa huduma kwa wanafunzi (ujuzi wa ushirikiano, kujitambua binafsi na kuimarisha umimi, utendaji wa kikundi).
- Mpango wa kupambana na uonevu utakadiriwa kila mwaka kwa misingi ya taarifa zilizokusanywa na mrejesho.